**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# MWONGOZO WA UDHIBITI WA UCHAFUZI WA MAZINGIRA UTOKANAO NA KELELE NA MITETEMO

*Septemba, 2021*

## YALIYOMO


**DIBAJI** .......... iii

**SHUKRANI** .......... iv

**VIFUPISHO YA MANENO** .......... v

**SURA YA KWANZA** .......... 1

**1.0 UTANGULIZI** .......... 1

- **1.1 Hali ya uchafuzi wa mazingira utokanao na kelele na mitetemo** .......... 2
- **1.2 Madhumuni ya Mwongozo** .......... 3
- **1.3 Umuhimu wa Kuandaa Mwongozo** .......... 3
- **1.4 Walengwa wa Mwongozo** .......... 3

**SURA YA PILI** .......... 4

**2.0 SHERIA NA SERA ZINAZOONGOZA UDHIBITI WA KELELE NA MITETEMO** .......... 4

**SURA YA TATU** .......... 7

**3.0 MUUNDO WA WADAU WA UTEKELEZAJI WA UDHIBITI KELELE NA MITETEMO** .......... 7

**SURA YA NNE** .......... 12

**4.0 HITIMISHO** .......... 12

**ORODHA YA NYARAKA ZILIZOREJEWA** .......... 14

# DIBAJI

Uchafuzi wa Mazingira unasababishwa na kelele na mitetemo ni miongoni mwa kero kubwa inayohatarisha afya na mustakabali wa maendeleo ya jamii katika maeneo mengi nchini.

Shirika la Afya Duniani (WHO) limebainisha kuwa kelele ni mojawapo ya vitu hatarishi katika maisha ya binadamu. Aidha kwa mujibu wa "European Environmental Agency" (EEA, 2018) kelele ni mojawapo ya kisababishi cha vifo vya mapema kwa watoto "Pre-mature death".

Changamoto ya kelele inachangiwa zaidi na kukua kwa shughuli za kiuchumi na kijamii ikiwemo matumizi mabaya ya teknolojia. Kwa siku za hivi karibuni, kelele zimeongezeka kwenye maeneo ya makazi na hivyo kusababisha matatizo ya kiafya kwa jamii ikiwemo kupoteza uwezo wa kusikia, matatizo ya uzazi, kupunguza umakini katika mafunzo, ajali na uwezo wa kawaida wa kusikilizana.

Vyanzo vikuu vya kero ya kelele ni pamoja na kumbi za starehe ikiwemo biashara za vileo (baa), vyombo vya usafiri na usafirishaji (magari, ndege, treni nk.), matumizi ya teknolojia zilizopitwa na wakati kwenye viwanda vikubwa na vidogo (Karakana za kuchomelea, ufyatuaji matofali, mashine za kusaga na kukoboa nafaka), majenereta, matangazo ya biashara kwenye makazi, shughuli za ujenzi, nyumba za ibada n.k.

Hivyo katika kukabiliana na changamoto ya kelele ni muhimu kuimarisha jitihada za pamoja na ushirikiano miongoni mwa Taasisi za Serikali na wadau ili kusimamia viwango vya kelele na mitetemo vilivyowekwa kwa mujibu wa Sheria.

Selemani S. Jafo (Mb.)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS**
**MUUNGANO NA MAZINGIRA**

## SHUKRANI


Kukamilika kwa Mwongozo huu wa Udhibiti wa Uchafuzi wa Mazingira utokanao na Kelele na Mitetemo ni matokeo ya jitihada za dhati za wadau mbalimbali wa usimamizi wa Mazingira hapa Nchini.

Napenda kutoa shukrani kwa timu ya wataalamu iliyoshiriki katika kuandaa Mwongozo huu. Timu hii iliundwa na wataalamu kutoka Ofisi ya Rais – TAMISEMI; Ofisi ya Makamu wa Rais; Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana na Ajira; Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto; Wizara ya Viwanda na Biashara; Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknologia: Wizara ya Mambo ya Ndani: Jeshi la Polisi: Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira, na Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA).

Vilevile, natoa shukrani zangu kwa Dkt. Andrew M. Komba - Mkurugenzi wa Mazingira, Ofisi ya Makamu wa Rais na Bi. Kemilembe Mutasa - Mkurugenzi Msaidizi wa Udhibiti wa Uchafuzi wa Mazingira kwa kuratibu uandaaji wa Mwongozo huu.

Mwisho, nawashukuru wadau wote waliotoa michango yao kwa namna moja ama nyingine katika kukamilisha Mwongozo huu unaolenga kuboresha usimamizi na udhibiti wa uchafuzi wa mazingira unaotokana na kelele na mitetemo


Mary N. Maganga
**KATIBU MKUU**
**OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

## VIFUPISHO YA MANENO

| | |
|---|---|
| **dBA** | Ni kielelezo cha kiwango cha kelele katika usikivu wa binadamu |
| **DCC** | Kamati za Ushauri za Wilaya |
| **EEA** | *European Environmental Agency* |
| **MUHAS** | Chuo Kikuu cha Tiba Muhimbili |
| **NEMC** | Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira |
| **OSHA** | Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi |
| **OR-TAMISEMI** | Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| **RCC** | Kamati za Ushauri za Mikoa |
| **SUA** | Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine |
| **TBS** | Shirika la usimamizi wa viwango Tanzania |
| **UDSM** | Chuo Kikuu cha Dar es Salaam |

# SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

Kelele ni sauti zilizozidi viwango zinazosababisha madhara kwa afya ya binadamu, wanyama na mazingira. Uchafuzi huu unatokana na kelele zisizo dhibitiwa pale zinapozalishwa na kusababisha athari za kiafya kwa jamii.

Shirika la Afya Duniani (WHO) limebainisha kelele kuwa ni mojawapo ya kisababishi cha madhara katika maisha ya binadamu. Aidha, kwa mujibu wa *"European Environmental Agency"* (EEA, 2018) kelele zimeainishwa kuwa mojawapo ya visababishi vya vifo vya mapema vya watoto *"Pre-mature death"* ambapo takwimu zinaonyesha takribani watoto 12,000 hufariki kila Mwaka katika Bara la Ulaya".

Katika nchi yetu changamoto ya kelele zinazozidi viwango vilivyoainishwa na *TBS* zinatokana na kukua kwa shughuli za kiuchumi na kijamii ikiwemo matumizi yasiyo sahihi ya teknolojia. Kwa siku za hivi karibuni, kelele zimeongezeka kwenye maeneo ya kazi na hivyo kusababisha matatizo ya kiafya ikiwemo kupoteza uwezo wa kusikia, matatizo ya uzazi, kupunguza umakini katika mafunzo, ajali na kupungua uwezo wa kusikilizana.

Vyanzo vikuu vya kelele hizi ni kumbi za starehe hasa biashara za vileo (baa), vyombo ya usafiri na usafirishaji (kama magari, ndege na treni), matumizi ya teknolojia zilizopitwa na wakati kwenye viwanda vikubwa na vidogo (Karakana za kuchomelea, ufyatuaji matofali, mashine za kusaga na kukoboa nafaka), majenereta, matangazo ya biashara mitaani, shughuli za ujenzi, nyumba za ibada n.k.

Sababu zinazopelekea uwepo wa changamoto hizi ni pamoja na usimamizi usioridhisha wa sheria mbalimbali zikiwemo Sheria ya Mipangomiji na Kanuni zake, Sheria ya Mazingira na Kanuni zake, Sheria ya Afya ya Jamii, Sheria ya Afya na Usalama Kazini, Sheria ya Baraza la Sanaa la Taifa na Sheria ya Usajili ya Jumuiya. Mapungufu haya yamesababisha shughuli za kimaendeleo kufanyika kinyume na matumizi ya ardhi yaliyopangwa kwenye maeneo husika na kutokuzingatiwa kwa masharti yanayotolewa kwenye vibali vya shughuli mbalimbali.

Nchini Tanzania, Kanuni za Usimamizi wa Mazingira *(Udhibiti wa kelele na mitetemo)* za mwaka 2015 zimeanisha viwango vinavyoruhusiwa katika maeneo ya makazi, biashara, viwanda na hospitali kwa afya ya jamii. Vilevile Sheria ya Usalama na Afya Mahala Pa Kazi namba 5 ya mwaka 2003 imeanisha viwango vya kelele vinavyoruhusiwa katika maeneo ya sehemu za kazi ambavyo haviruhusiwi kuzidi 85dBA.

## 1.1 Hali ya uchafuzi wa mazingira utokanao na kelele na mitetemo

Kutokana na ongezeko la watu duniani na shughuli za kiuchumi na kijamii, kelele zimeendelea kuongozeka kwenye makazi ya watu na maeneo ya biashara na hivyo kusababisha madhara mbalimbali kwa binadamu na mazingira. Madhara hayo ni pamoja na kupoteza usikivu (*hearing loss*); kuondosha utulivu; kupunguza ufanisi wa kazi; kuzuia watu wasipate usingizi; athari za kisaikolojia kwa watoto; magonjwa ya moyo; usumbufu kwa wagonjwa; kupunguza umakini wakati wa kujisomea na kero kwa jamii.

Katika siku za hivi karibuni Mamlaka ya Udhibiti zimeendelea kupokea taarifa juu ya matukio yanayohusiana na kelele na mitetemo. Katika kipindi cha mwezi Januari hadi Aprili 2021 jumla ya malalamiko 20 yaliripotiwa katika Jiji la Dodoma na malalamiko 8 katika Jiji la Mwanza. Maeneo yaliyoongoza kwa kulalamikiwa ni kumbi za starehe na burudani na nyumba za Ibada. Aidha, ili kubaini ukubwa wa tatizo la uchafuzi wa mazingira utokanao na kelele na mitetemo tafiti mbalimbali zimefanyika. Miongoni mwa tafiti hizo ni pamoja na:

i. Utafiti wa kiwango cha kilele katika mwaka wa 2019, uliofanywa na Chuo Kikuu cha Tiba Muhimbili (MUHAS) kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) katika viwanda vya nguo vilivyopo Dar Es Salaam na kubaini kuwa zaidi ya asilimia 58 ya wafanyakazi wamepoteza usikivu.
ii. Utafiti wa kiwango cha kilele katika mwaka wa 2014, uliofanywa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) katika mashine 41 za kusaga nafaka kwenye miji ya Dar Es Salaam na Morogoro ambao ulionyesha kiwango cha kelele kufikia 103 dBA juu ya kiwango cha 70 dBA ambacho kimeruhusiwa;
iii. Utafiti wa kiwango cha kilele katika mwaka wa 2010, uliofanywa na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) katika hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa iringa ambapo kiwango cha kelele kilifikia 63 dBA juu ya kiwango kilichowekwa na TBS cha 35dBA;

iv. Utafiti wa kiwango cha kilele katika mwaka wa 2009 uliofanywa na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) katika migahawa *(Restaurants)* 7 iliyo karibu na makazi ya watu ulionyesha kuwa kelele zimezidi na kufikia 73 dBA tofauti na kiwango kilichowekwa na TBS cha 55 dBA;

## 1.2 Madhumuni ya Mwongozo

Mwongozo huu unalenga kuboresha usimamizi na udhibiti wa uchafuzi wa mazingira unaotokana na kelele na mitetemo kwa kuanisha namna ambavyo wadau mbalimbali watashiriki katika kupunguza kero zitokanazo na kelele na mitetemo nchini.

Malengo Mahsusi ya Mwongozo huu ni pamoja na:-

i). Kuainisha wajibu wa kila mdau katika kudhibiti kelele na mitetemo.

ii). Kubainisha na kupendekeza njia na mifumo itakayosaidia kupunguza kero zitokanazo na kelele na mitetemo.

## 1.3 Umuhimu wa Kuandaa Mwongozo

Kukosekana kwa Mwongozo mahsusi unaoelekeza majukumu kwa kila mdau kumechangia kuongezeka kwa kero ya uchafuzi wa mazingira utokanao na kelele na mitetemo katika jamii. Aidha, kuandaliwa kwa Mwongozo huu kunaweka mfumo utakaowezesha kudhibiti changamoto za kelele na mitetemo katika jamii.

## 1.4 Walengwa wa Mwongozo

Mwongozo huu unalenga kutumiwa na wadau mbalimbali wakiwemo wamiliki wa kumbi za starehe na burudani; Wamiliki wa Viwanda; Wizara na Taasisi; Mamlaka za Serikali za Mitaa; na Jamii kwa ujumla.

# SURA YA PILI

## 2.0 SHERIA NA SERA ZINAZOONGOZA UDHIBITI WA KELELE NA MITETEMO

Udhibiti wa kelele na mitetemo nchini unasimamiwa na Sheria mbalimbali zikiwemo Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 pamoja na Kanuni za Usimamizi wa Mazingira (Udhibiti wa Kelele na Mitetemo) za Mwaka 2015; Sheria ya Usalama Kazini ya Mwaka 2003; Sheria ya Afya ya Jamii ya Mwaka 2009; Sheria ya Jumuiya [Sura ya 337 Marejeo ya 2002]; Sheria ya Baraza la Sanaa la Taifa [Sura 204 Marejeo ya 2002] na Kanuni za Baraza la Sanaa la Taifa za Mwaka 2018; Sheria ya Ardhi [sura 113 Marejeo ya Mwaka 2019] na Sheria ya Mipango Miji ya Mwaka 2007 pamoja na Kanuni zake za Mwaka 2018.

Sheria na Kanuni hizi zimeelekeza shughuli zote zenye madhara zifanyike mbali na makazi ya watu na hivyo shughuli zenye kelele kufanyika mbali na makazi ya watu ili kupunguza madhara kwa afya ya binadamu na mazingira.

### i) Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004

Kifungu cha 106 (6) cha Sheria hii kimeanisha ni kosa la kupiga kelele kuzidi viwango vilivyoruhusiwa. Vilvile kifungu cha 106 (5) cha Sheria hii kinakataza kupiga kelele kinyume na viwango vilivyoruhusiwa. Sheria na Kanuni zimeainisha viwango vya sauti vinavyoruhusiwa kwenye maeneo na shughuli mbalimbali za uzalishaji mali kwa kuzingatia matumizi ya Ardhi husika na kuweka kosa la jinai kwa anayekiuka viwango vilivyoainishwa. Kanuni hizi zinatoa majukumu kwa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira, Maafisa Mazingira wa Serikali za Mitaa na Wakaguzi wa Mazingira katika kusimamia Kanuni hizi.

### ii) Sheria ya Afya ya Jamii ya mwaka 2009

Kwa kuzingatia changamoto hizo suala la udhibiti wa kelele limepewa umuhimu na kuwekwa kwenye Sheria ya Afya ya Jamii ya mwaka 2009 kifungu cha 53 (W) ambacho kinahusu "udhibiti wa kelele" kama sehemu ya "***Nuisance***". Kadhalika vifungu 53 - 60 vinatoa nguvu kwa mamlaka za Serikali za Mitaa, Mganga Mkuu wa Serikali, Mganga Mkuu wa Mkoa, Mganga Mkuu wa Wilaya na Afisa Afya Mazingira ambao ni "Authorized officers" kuondosha chukizo, au hatari, kutoa ilani au maelekezo, kufunga biashara au huduma iliyo na chukizo.

Kwa kuzingatia sheria hizi Mamlaka ya Serikali za Mitaaa kupitia wataalamu wa Afya Mazingira hufanya usajili, ukaguzi wa majengo, viwanda na nyumba za biashara (*Inspection of premises*) na kutoa ilani ya kusitisha shughuli zinazozalisha au kupelekea kelele zilizopitiliza.

### iii) Sheria ya Mipango Miji ya Mwaka 2007

Udhibiti wa kelele umepewa umuhimu kwa kuandaa Kanuni zinazoelekeza uendelezaji ardhi kufanyika kwenye maeneo yaliyotengwa kutokana na aina ya shughuli. Aidha Kanuni ya 7 (3) ya Kanuni za Mipango Miji (Maombi ya Idhini ya Uendelelezaji) za Mwaka 2018 zinaelekeza kuhakikisha kuwa uendelezaji wowote hauleti kero yoyote (ikiwemo kelele) inayoweza kuhatarisha afya ya jamii. Aidha, waraka wa Kitaalamu Na. 1 wa mwaka 2018 kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi unaelekeza kuwa mabadiliko ya matumizi ya ardhi yanayosababisha kero/adha kwa njia za kelele, vumbi, moshi, harufu mbaya, n.k katika makazi ya watu hayataruhusiwa.

### iv) Sheria ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1982

Kupitia Sheria hii udhibiti wa kelele umepewa umuhimu kwa kuandaa Kanuni za Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) (Udhibiti Uendelezaji) za mwaka 2008 zinazoelekeza ujenzi wowote katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ni lazima upate kibali cha ujenzi ili kuwa na miji endelevu na kulinda afya ya jamii.

### v) Sheria ya Jumuiya [Sura ya 337 Marejeo ya 2002]

Usajili wa jumuiya za kidini ulianza nchini chini ya Sheria ya Jumuiya Sura 337. Sheria hii imeangalia usalama wa wananchi na kuzitaka jumuiya zote za dini zilizosajiliwa kutunza amani miongoni mwao na kwa jamii nzima. Kifungu cha 14(a) cha sheria ya Jumuiya Sura 337 kinazitaka jumuiya zote za dini nchini kuzingatia sheria mbalimbali zilizopo nchini. Jumuiya isiyozingatia matakwa ya kifungu hiki haiwezi kusajiliwa na iwapo imesajiliwa inaweza kufutiwa usajili.

### vi) Sheria ya Baraza la Sanaa la Taifa [Sura 204 Marejeo ya 2002] na Kanuni za Baraza la Sanaa la Taifa za Mwaka 2018.

Kanuni zimeanisha maeneo mawili mahsusi katika udhibiti wa kelele ikiwa ni pamoja na;

1. Kutoa vibali vya matukio ya sanaa kwa mujibu wa masharti ya Kanuni ya 52 (iv) na tukio hilo liendeshwe kwenye maeneo bila kubughudhi jamii.

2. Aidha Kanuni ya 55 (2) na 57 zimeanisha madaraja ya maeneo ya kumbi za starehe;
    a. Daraja 'A' ni kumbi zisizotoa sauti nje zinatumika masaa 24

b. Daraja 'B' ni maeneo maalum kwa kazi za sanaa na yametengwa maalumu kwa shughuli hiyo zinatumika kuanzia saa 10:00 jioni mpaka Saa 06:00 usiku, siku za Jumatatu (3) hadi Ijumaa na weekend na Siku Kuu hadi saa 8:00 usiku.
c. Daraja 'C' kumbi zisizozuia sauti kutoka nje na zimejengwa kwenye makazi ya watu zinatumika kuanzia saa 10:00 jioni hadi saa 3:00 usiku kwa siku zote za juma

# SURA YA TATU

## 3.0 MUUNDO WA WADAU WA UTEKELEZAJI WA UDHIBITI KELELE NA MITETEMO

Mwongozo huu unatoa maelekezo mahsusi ya namna ya kusimamia na kudhibiti kelele na mitetemo kwa makundi mbalimbali ikiwa ni pamoja na Wizara, Taasisi, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Viwanda, Sekta ya Ujenzi, Kumbi za Starehe na Burudani na Jamii. Katika kutekeleza Mwongozo huu wadau watafanya yafuatayo:

### 3.1 Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

Katika kuhakikisha kelele na mitetemo zinadhibitiwa, TAMISEMI itafanya yafuatayo:

a. Kuhakikisha suala la kelele na mitetemo linakuwa agenda ya kudumu katika vikao vya Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.
b. Kupokea taarifa ya robo mwaka ya utekelezaji wa usimamaizi na udhibiti wa uchafuzi wa mazingira utakanao na kelele na mitetemo.
c. Kuchukua hatua za kinidhamu Kwa Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo hazijatekeleza ipasavyo shughuli za udhibiti wa kelele na mitetemo.

### 3.2 Ofisi ya Makamu wa Rais – Dhamana ya Mazingira

Katika kuhakikisha kelele na mitetemo zitokanazo na shughuli mbalimbali zinadhibitiwa, Ofisi ya Makamu wa Rais itafanya yafuatayo:

a. Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mwongozo.
b. Kupokea taarifa za robo mwaka kuhusu utekelezaji wa Mwongozo kutoka OR-TAMISEMI na NEMC.
c. Kufanya mapitio ya Mwongozo kila baada ya miaka mitatu (3) au itakapobidi.

### 3.3 Wizara yenye dhamana ya Afya

Katika kuhakikisha kelele na mitetemo zitokanazo na shughuli mbalimbali zinadhibitiwa, Wizara ya Afya itafanya yafuatayo:

a. Kufanya tafiti ili kubaini athari mbalimbali za kiafya zitokanazo na kelele na mitetemo
b. Kuweka utaratibu endelevu wa upimaji usikivu ili kubaini na kutibu walioathirika
c. Kushirikiana na mamlaka zingine kukagua maeneo yote mara kwa mara kwa lengo la kudhibiti vyanzo vya kelele
d. Kutoa elimu juu ya athari zitokanazo na kelele na mitetemo
e. Kuitisha vikao vya pamoja vya kisekta kujadili changamoto zitokanazo na kelele na mitetemo

### 3.4 Wizara yenye dhamana ya Sanaa na Michezo

Katika kuhakikisha kelele na mitetemo katika maeneo mbalimbali, Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo itafanya yafuatayo:

a. Kufuatilia utekelezaji wa masharti ya leseni za burudani.

b. Kuhamasisha vyombo vya habari kushiriki katika kuhabarisha jamii juu ya hatua za kuchukua katika kushughulikia kero zitokanazo na kelele na mitetemo.
c. Kuhabarisha umma kuhusu athari za kelele na mitetemo.
d. Kushiriki katika vikao vya kufanya tathmini na kutoa maamuzi juu ya uthibiti wa kelele na mitetemo katika jamii.

### 3.5 Wizara yenye dhamana ya Elimu

Katika kuhakikisha kelele na mitetemo zitokanazo na shughuli za Elimu zinadhibitiwa, Wizara ya Elimu itafanya yafuatayo:

a. Kufanya tafiti mbalimbali zinalenga kudhibiti uchafuzi wa mazingira utokanao na kelele na mitetemo
b. Kufanya kaguzi kuhakikisha shule zinakuwa kwenye mazingira yasiyo na kelele.
c. Kuandaa mitaala katika ngazi mbalimbali za elimu inayohusu uchafuzi wa mazingira utokanao na kelele na mitetemo

### 3.6 Taasisi za Serikali

#### i). Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC)

Katika kuhakikisha kelele na mitetemo zitokanazo na shughuli mbalimbali zinadhibitiwa, Baraza litafanya yafuatayo:

a. Kuendelea na ukaguzi wa maeneo ya biashara na kutoa maelekezo mbalimbali ikiwemo Amri na Ilani za kudhibiti kelele.
b. Kuainisha na kutangaza maeneo ambayo kelele haziruhusiwi (Noise Control Zone).
c. Kusimamia uainishaji wa ramani za maeneo yenye kelele zilizopitiliza na kuandaa Mkakati wa udhibiti.
d. Kufanya tafiti za mara kwa mara kubaini hali ya uchafuzi wa mazingira utokanao na kelele na mitetemo.
e. Kutoa elimu kwa jamii na maafisa mazingira kuhusu majukumu yao katika udhibiti wa kelele na mitetemo.
f. Kupokea taarifa za malalamiko yanayohusu kelele na mitetemo.

#### ii). Mamlaka ya Afya na Usalama Mahala Pa Kazi (OSHA)

Mamlaka ya Afya na Usalama Mahala Pa Kazi katika kudhibiti kelele na mitetemo litafanya yafuatayo:

a. Kufanya ukaguzi kwenye maeneo ya kazi ili kubaini athari zitokanazo na kelele na kutoa ushauri kwa mwajiri namna bora ya kuzuia kelele zisilete athari za kiafya kwa wafanyakazi na jamii inayozunguka eneo la husika.
b. Kupima afya za wafanyakazi ili kubaini athari za kiafya kutokana na kelele na mitetemo.
c. Kutoa elimu na mafunzo kuhusu athari zinazotokana na kelele na mitetemo.
d. Kuweka mfumo wa kupokea taarifa za malalamiko ya wafanyakazi yanayohusu kelele na mitetemo

#### iii). Shirika la Viwango Tanzania (TBS)

Katika kudhibiti changamoto ya kelele na mitetemo, Shirika la Taifa la Viwango litafanya yafuatayo:

a. Kusimamia viwango vya ubora katika kudhibiti uchafuzi wa mazingira utokanao na kelele na mitetemo.
b. Kufanya kaguzi za mara kwa mara kwa ajili ya kuhakikisha vifaa vinavyotumika kama vinakidhi viwango.

#### iv). Jeshi la Polisi

Katika kudhibiti changamoto ya kelele na mitetemo, Jeshi la Polisi litafanya yafuatayo:

a. Kushirikiana na Baraza la Hifadhi ya Mazingira na Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini kukagua vyombo vya usafiri ili kubaini uchafuzi wa mazingira utokanao na kelele na mitetemo
b. Kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mtaa na Baraza la Hifadhi ya Mazingira katika kudhibiti uchafuzi wa mazingira utokanao na kelele na mitetemo.
c. Kufuatilia malalamiko yanayohusu uchafuzi utokanao na kelele na mitetemo yanafanyiwa kazi.
d. Kutoa elimu kwa jamii juu ya utekelezaji wa Kanuni ya udhibiti wa kelele na mitetemo bila shuruti

#### v). BASATA.

Katika kudhibiti changamoto ya kelele na mitetemo, BASATA itafanya yafuatayo:

a. Kusimamia vibali vya matukio ya sanaa na burudani ili kuhakikisha kuwa vinatumika kulingana na masharti ya vibali husika.
b. Kutoa elimu juu ya athari zitokanazo na kelele na mitetemo.
c. Kushiriki katika vikao vya kufanya tathmini na kutoa maamuzi juu ya uthibiti wa kelele na mitetemo katika jamii.

### 3.7 Tawala za Mikoa

#### i) Sekretarieti ya Mkoa

Katika kudhibiti changamoto ya kelele na mitetemo, Sekretarieti ya Mkoa itafanya yafuatayo:

a. Kuhakikisha suala la kelele na mitetemo linakuwa agenda ya kudumu katika vikao vya Kamati za Ushauri za Mikoa (RCC)
b. Kusimamia utekelezaji wa agenda ya kelele na mitetemo maeneo yao ya kazi
c. Kuratibu utekelezaji wa shughuli za kelele na mitetemo kwa Serikali za Mitaa
d. Kutoa taarifa za robo mwaka kuhusu utekelezaji wa Mwongozo.

#### ii) Ofisi za Wakuu wa Wilaya

Katika kuhakikisha kelele na mitetemo zitokanazo na shughuli mbalimbali zinadhibitiwa, Sekretarieti ya Wilaya itafanya yafuatayo:

a. Kuhakikisha suala la kelele na mitetemo linakuwa agenda ya kudumu katika vikao vya Kamati za Ushauri Wilaya (DCC).
b. Kusimamia utekelezaji wa agenda ya kelele na mitetemo katika ngazi za Serikali za Mitaa.
c. Kutoa taarifa za robo mwaka kuhusu utekelezaji wa Mwongozo.

### 3.8 Mamlaka za Serikali za Mitaa

Katika kudhibiti changamoto ya kelele na mitetemo, Mamlaka za Serikali za Mitaa zitafanya yafuatayo:

a. Kusimamia utekelezaji wa Sheria kwa anayekiuka masharti ya kibali husika.
b. Kuhakikisha utoaji wa vibali na leseni katika maeneo ya starehe na burudani unahusisha jamii katika eneo husika kwa kufanya vikao na jamii kuhusu shughuli zinazoombewa kibali au leseni.
c. Kuchukua hatua kwa anayekiuka masharti ya leseni/vibali.
d. Kuhakikisha suala la kelele na mitetemo ni moja ya agenda katika vikao vya Kamati za Mitaa na Mikutano ya wananchi.
e. Kufanya kaguzi za mara kwa mara kwenye vyombo vya usafiri katika vituo vya mabasi, maegesho ya magari, na karakana za kutengeneza magari.
f. Kuhakikisha ushiriki wa wataalam kwenye vikao vya mabadiliko ya matumizi ya ardhi.

### 3.9 Viwanda

Katika kudhibiti changamoto ya kelele na mitetemo viwanda vitafanya yafuatayo:

a. Kila kiwanda kihakikishe kina Mpango unaoonesha namna ya kudhibiti uchafuzi wa mazingira utokanao na kelele na mitetemo.
b. Kuhakikisha uwepo wa vizuia sauti (*Sound proof*).
c. Kufanya vikao vya mara kwa mara na jamii inayozunguka eneo la kiwanda ili kuwafahamisha hatua mbalimabli zinazochukuliwa katika kushughulikia kero zinazojitokeza.
d. Kuhakikisha kuwepo kwa namba ya simu ya bure itakayopatikana masaa 24 kwa ajili ya kupokea malalamiko.

### 3.10 Sekta ya Ujenzi

Katika kudhibiti changamoto ya kelele na mitetemo, Sekta ya ujenzi itafanya yafuatayo:

a. Kuhakikisha kila eneo la ujenzi linakuwa na mpango wa kudhibiti uchafuzi wa mazingira utokanao na kelele na mitetemo.
b. Kuhakikisha nakala ya Mpango wa namna ya kudhibiti uchafuzi wa mazingira utokanao na kelele na mitetemo inawasilishwa kwenye Ofisi za Kata na Mtaa.
c. Kufanya vikao vya mara kwa mara na jamii inayozunguka eneo la ujenzi ili kuwafahamisha hatua mbalimabli za mwenendo wa mradi na hatua zinazochukuliwa katika kushughulika kero zinazojitokeza.
d. Kuwepo kwa namba ya simu ya bure itakayopatikana masaa 24 kwa ajili ya kupokea malalamiko.

### 3.11 Kumbi za Starehe na Maeneo ya Burudani

Katika kudhibiti changamoto ya kelele na mitetemo, Sekta hii itafanya yafuatayo:

a. Kumbi za starehe/burudani ziwe na vipima kelele na vizuia sauti
b. Mmiliki wa kumbi za starehe/burudani ahakikishe anawasilisha leseni au kibali cha kuruhusu shughuli anayofanya katika Ofisi ya Serikali ya Mtaa ya eneo husika.
c. Kuwepo kwa namba ya simu ya bure itakayopatikana masaa 24 kwa ajili ya kupokea malalamiko.
d. Kubandika nakala ya kibali kwenye kumbi.

### 3.12 Taasisi za kidini/Nyumba za ibada

Katika kudhibiti changamoto ya kelele na mitetemo, Taasisi za kidini zitafanya yafuatayo:

a. Kuendesha shughuli za ibada kwa kuzingatia matumizi ya ardhi yaliyopangwa katika eneo husika,
b. Kuhakikisha nyumba za ibada zinazingatia Sheria na Kanuni za Usimamizi wa Mazingira (Udhibiti wa Kelele na Mitetemo) za 2015 katika kuendesha shughuli zao.
c. Kudhibiti kelele kutoka kwenye nyumba za ibada kwa kuzingatia viwango vya kelele vinavyoruhusiwa.
d. Kupata kibali kutoka Mamlaka husika pale watakapo lazimika kufanya shughuli itakayopelekea kuwa na kelele juu ya kiwango kinachoruhusiwa.

### 3.13 Jamii

Katika kudhibiti changamoto ya kelele na mitetemo, Jamii itafanya yafuatayo:

a. Kutoa taarifa za uendelezaji unaofanyika katika maeneo yao ambao unaweza kuwa chanzo cha kelele na mitetemo kwa Ofisi za Serikali za Mitaa.
b. Kuhakikisha agenda ya kelele na mitetemo inakuwepo kwenye mikutano ya wananchi.
c. Kutoa taarifa kuhusu kero ya kelele na mitetemo kwa Mamlaka husika(NEMC/Serikali ya Mtaa/Ofisi ya Kata)

# SURA YA NNE

## 4.0 HITIMISHO

Kelele na Mitetemo ni miongoni mwa changamoto inayoongezeka kwa kasi kutokana na ukuaji wa miji. Hivyo, Kila mdau anao wajibu wa kutimiza majukumu yaliyoainishwa katika Mwongozo huu. Aidha, wadau wote wakiwa ni pamoja na wazalishaji wa kelele na mitetemo wanahimizwa kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa Mwongozo huu ili kulinda afya ya binadamu na mazingira kwa maendeleo endelevu.

## Kiambatisho Na. I:

*Jedwali Na. I linaonesha viwango vilivyoruhusiwa kwenye eneo lenye matumizi mchanganyiko ya ardhi kama ifuatavyo.*

| **Mahali/Eneo** | **Kiwango kinachoruhusiwa** | |
|---|---|---|
| | **Mchana** | **Usiku** |
| *Viwandani* | *70 dBA* | *60 dBA* |
| *Makazi* | *50 dBA* | *35 dBA* |
| *Makazi na viwanda vidogovidogo* | *60 dBA* | *50 dBA* |
| *Maeneo ya makazi, biashara na burudani* | *55 dBA* | *45 dBA* |
| *Maeneo ya hospitali, taasisi za elimu, kumbi za mikutano, makazi ya wazee na maeneo ya mapumziko* | *45 dBA* | *35dBA* |

## ORODHA YA NYARAKA ZILIZOREJEWA


1. European Environmental Agency (EEA), (2018).
2. *WHO, (2018). WHO Environmental Noise Guidelines for the European Region.*
3. Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004.
4. Sheria ya Usalama Kazini ya Mwaka 2003.
5. Sheria ya Afya ya Jamii ya Mwaka 2009.
6. Sheria ya Jumuiya [Sura ya 337 Marejeo ya 2002].
7. Sheria ya Baraza la Sanaa la Taifa [Sura 204 Marejeo ya 2002]
8. Sheria ya Ardhi [sura 113 Marejeo ya Mwaka 2019]
9. Sheria ya Mipango Miji ya Mwaka 2007
10. Kanuni za Baraza la Sanaa la Taifa za Mwaka 2018;